



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA AFYA

BARAZA LA WATAALAMU WA MAABARA



Tovuti: www.hlpc.go.tz

• TANGAZO

**KUFUNGULIWA KWA DIRISHA LA MAOMBI YA UTARAJALI (INTERNSHIP)-
AWAMU YA PILI**

Baraza la Wataalam wa Maabara linachukuwa nafasi hii kuwajulisha Wataalamu wote wanaotarajia kufanya maombi ya utarajali (internship) kwa ngazi ya Shahada (Bachelor Degree) kuwa dirisha la maombi ya utarajali kwa awamu ya pili mwaka 2022/2023 litafunguliwa rasmi tarehe **03 Novemba 2022 saa 4:00 Asubuhi na litafungwa 04 Novemba saa 9:30 alasiri**

Waombaji wote wanatakiwa kuzingatia maelekezo yafuatayo;

1. Wawe wameshafanya maombi ya usajili wa awali (Provision Registration) kwenye mfumo wa-usajili (HPRS) kabla ya dirisha la usajili kufungwa
2. Kuwa na taarifa za Benki ni lazima
3. Kila kituo cha utarajali kina idadi ya Watarajali takiwa, hivyo kila mtarajali atatakiwa kuwahi nafasi katika kituo anachokihitaji kabla ya nafasi kujaa
4. Kabla ya dirisha kufungwa, mfumo utamruhusu mtarajali kubadili kituo alichoomba kwenda kituo kingine kama kituo anachokihitaji kitakuwa na nafasi (hakijajaa). Baada ya dirisha kufungwa hakutakuwa na nafasi ya kubadilisha kituo cha utarajali.
5. Kikao cha Watarajali wanaotegemea kuomba vituo vya utarajali katika tarehe tajwa hapo juu kitafanyika siku ya Jumamosi ya tarehe **05 Novemba 2022 saa 2:30 Asubuhi** katika **Chuo kikuu cha Dodoma, Kitivo cha Tiba (Faculty of Medicine & Dentistry)** kwenye ukumbi wa CHS-Library

Upatapo tangazo hili mtaarifu mwenzako.

Imetolewa na

Msajili

Baraza la Wataalamu wa Maabara

